**HOTUBA YA KATIBU MTENDAJI WA BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI WAKATI WA KILELE CHA MAONESHO YA MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI KATIKA UWANJA WA BOMBADIA, MKOA WA SINGIDA TAREHE 14 SEPTEMBA, 2024**

- ***Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati;***
- ***Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu;***
- ***Mheshimiwa***
- ***Mheshimiwa Halima Dendego, Mkuu wa Mkoa wa Singida***
- ***Dkt. Fatuma Mganga, Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida;***
- ***Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida;***
- ***Viongozi mbalimbali wa Vyama vya Siasa;***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;***
- ***Ndugu Condrad Milinga, Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu;***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;***
- ***Viongozi wa Madhehebu mbalimbali ya Dini;***
- ***Waheshimiwa Madiwani;***
- ***Wakuu wa Taasisi zinazosimamia Mifuko na Programu za Uwezeshaji;***
- ***Wakuu wa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi;***
- ***Wajasiriamali walionufaika na Mifuko na Programu za Uwezeshaji na ambao hawajanufaika;***
- ***Ndugu Wananchi na Wadau wote wa Uwezeshaji, bila kusahau walioko kwenye mabanda ya Maonesho;***
- ***Wanahabari;***
- ***Wageni Waalikwa;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kutufikisha siku ya leo ambapo tunahitimisha maonesho yetu ya Saba ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji. Pili ninapenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kuwa na sisi leo hapa. **Tunakushukuru sana**.

Nawashukuru pia wote walioalikwa na kuweza kuja kushuhudia Kilele cha Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji wakiwemo Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Taasisi mbalimbali katika sekta ya umma na sekta binafsi, wajasiriamali, wanahabari na wananchi wote kwa ujumla wenu.Tunatambua kuwa nyote mnayo majukumu mengi mliyopanga kuyafanya siku ya leo lakini pamoja na hayo mmeweza kukubali mwaliko wetu na kuja kushiriki katika Kilele cha Maonesho haya.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Kipekee napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wadhamini wa Maonesho haya ya Saba ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji kwa michango yao wa hali na mali na kuwezesha kufanikisha Maonesho haya. ***Tunawashukuru sana kwa Udhamini huu.***

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Kabla ya Uhuru wananchi hawakushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi kutokana na vikwazo vya kiuchumi. Baada ya Uhuru mwaka 1961, wananchi walipata madaraka ya kisiasa lakini sehemu kubwa ya uchumi

bado ilibaki mikononi mwa wageni na baadhi ya Watanazania. Kutokana na hali hii, Serikali ilitangaza Azimio la Arusha mwaka 1967. Pamoja na kutangazwa kwa Azimio la Arusha, bado hali ya ushiriki wa Watanzania kwenye shuhuli za kiuchumi ilikuwa ndogo kutokana na: ukosefu wa mitaji; ukosefu wa ujuzi na uzoefu vikichochewa na upungufu katika elimu; ukosefu wa dhamana ya mikopo; ukosefu wa masoko ya uhakika au uwezo wa kuingia katika masoko yenye ushindani; na ushirika hafifu na ukosefu wa sauti ya pamoja ya makundi mbalimbali ya wananchi katika kusimamia maslahi yao.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Kutokana na ushiriki mdogo wa watanzania na changamoto zilizokuwa zikiwakabili Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa lengo la kujenga uchumi na kupunguza mzunguko wa umaskini kwa wananchi. Jitihada hizo ni pamoja na:-

> Kuanzisha mifuko na programu za uwezeshaji kwa lengo la kutoa mikopo na dhamana ya mikopo kwa wananchi kwa masharti nafuu. Mifuko na programu za uwezeshaji zinatoa huduma zinazohusu sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya mawasiliano, nishati, kilimo, biashara, afya, ujenzi, sanaa, utamaduni, mifugo, michezo, misitu, maji, mazingira, viwanda, utalii, elimu, nyumba na ardhi.

Kwa upande wa mifuko na programu za uwezeshaji zinatoa mikopo na dhamana ya mikopo, zimewezesha wafanyabiashara wadogo na kati kupata huduma za mikopo na dhamana ili kuanzisha na kukuza biashara.

. Hadi Juni, 2024, kuna jumla ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji 72 ambazo zimewezesha huduma za mikopo, dhamana na ruzuku kwa

wananchi. Kati ya mifuko na programu hizo, mifuko na proramu 65 zinamilikiwa na Serikali na mifuko na programu 7 zinamilikiwa na taasisi za sekta binafsi. Kati ya mifuko na programu 72 zilizopo, mifuko 18 inatoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa, mifuko 7 inatoa dhamana za mikopo, mifuko 33 inatoa ruzuku na programu za uwezeshaji 14.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Kutokana na changamoto ya kutofahamika kwa mifuko hii, Baraza kwa kushirikiana na Mikoa pamoja na Mifuko ya Uwezeshaji imekuwa ikifanya maonesho katika kanda mbalimbali kwa lengo la kujenga uelewa wa Mifuko hii kwa wananchi. Maonesho haya yalianza kufanyika mwaka 2017 ambayo hufanyika kikanda. **Maonesho ya Kwanza,** yalifanyika mwaka 2017 katika Kanda hii hii ya Kati iliyohusisha mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora ambapo yalifanyika katika Mkoa wa Dodoma; **Maonesho ya Pili,** yalifanyika mwaka 2018 katika Kanda ya Nyanda za Juu iliyohusisha mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Ruvuma na Songwe; **Maonesho ya Tatu,** yalifanyika Mwaka 2019 katika Kanda ya Ziwa na yalihusisha mikoa ya Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu na Shinyanga na **Maonesho ya Nne,** yalifanyika mwaka 2021 katika Kanda ya Kaskazini yahusisha mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga. **Maonesho ya Tano,** yalifanyika mwaka 2022 katika Kanda ya Mashariki ambayo imehusisha mikoa ya Dar Es Salaam, Pwani, Morogoro, Lindi na Mtwara, na haya ni **Maonesho ya Sita** yalifanyika katika kanda ya Magharibi na kuhusisha Mikoa ya Kigoma na Katavi.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Ili kuifanya mifuko na programu hizo zifahamike pia kwa Kanda hii na kusaidia wananchi kunufaika nayo, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana Ofisi ya Mkoa wa Singida na Taasisi zinazosimamia mifuko na programu za uwezeshaji imeandaa Maonesho haya ambapo kwa mwaka 2024 ni Maonesho ya saba yakiwa na Kaulimbiu:***SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA UNUFAIKE NA FURSA ZA UWEZESHAJI***. Maonesho haya yamefanyika katika kanda hii ya Kati na kuhusisha Mikoa ya Singida, Tabora na Dodoma na Mikoa ya Shinyanga, Manyara na Dar es Salaam imeweza kushiriki pia. Maonesho haya yalianza tarehe 8 na leo ni kilele chake tarehe 14 mwezi Septemba mwaka 2024.

Katika Maonesho haya, Taasisi zinazosimamia mifuko na programu za uwezeshaji za Serikali na za sekta binafsi zimeshiriki na kutangaza vigezo, sifa, masharti, taratibu kwa walengwa wa mikopo, dhamana na ruzuku ili kuleta uelewa na kuonesha jinsi mifuko na programu hizo zilivyobadilisha maisha ya wananchi.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Jitihada nyingine ambazo zimechukuliwa na Serikali katika kuwawezesha wananchi kwenye shughuli za kiuchumi na kupunguza mzunguko wa umaskini ni pamoja na:-

(i) Kutekeleza Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati *(SANVN Viwanda Scheme)* kwa lengo la kutoa fursa kwa Watanzania kupata mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo na vya kati hususan vilivyochakata mazao ya kilimo na

mifugo. Mpaka sasa mpango huo umewezesha mikopo yenye jumla ya thamani ya **Shilingi Bilioni 5.6** kwa **miradi 79** katika **mikoa 13**. Mikoa hiyo ni pamoja na: **Mwanza; Arusha**; **Dar Es Salaam**; **Kilimanjaro**; **Mbeya**; **Geita**; **Dodoma**; **Shinyanga** ; **Iringa**; **Njombe**; **Singida**; **Pwani** na **Rukwa**.

(ii) Kuanzisha vituo vya uwezeshaji kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi wa mwaka 2020 Ibara ya 26 (K). Nia ya Serikali ni kuhakikisha huduma za kuwawezesha wananchi kiuchumi zinapelekwa karibu na wananchi. Huduma hizi ni pamoja na: mikopo, mafunzo, urasimishaji wa biashara, ujuzi wa wafanyabiashara, uongezaji thamani ya mazao, elimu ya kodi na upatikanaji wa masoko. Hadi Juni, 2024 jumla ya vituo vya uwezeshaji 25 vimeanzishwa katika mikoa 11 ya Shinyanga (Vituo 3), Geita (Vituo 2), Singida, Rukwa, Kigoma (Vituo 6) na Dodoma (Vituo 7), Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Katavi na Tanga. Na baadhi ya Mifuko hii imeweka huduma katika baadhi ya vituo hivi na kwa mkwa awa fedha 2023/2024 vituo hivi viliwezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 6.1** kwa **wanufaika 1,497.** Niendelee kutoa wito kwa Mifuko ya Uwezeshaji na taasisi nyingine wezeshi kuendelea kuweka huduma zenu katika vituo hivi.

(iii) Na kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025 tunapenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha Baraza kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Uwezeshaji Mikoani ijulikanayo kama **IMARISHA UCHUMI NA MAMA SAMIA (IMASA).** Programu hii itatekelezwa Mikoani ikiwa chini ya Wakuu wa Mikoa kwa kuibua

vipaumbele vya Uwezeshaji Mikoani na kuja na Program makhsusi kwa kila Mkoa kwa kuzingatia, uhitaji, fursa na program zingine za Serikali zilizopo kama 30% ya Manunuzi ya Umma, Mikopo ya 10%, n.k hii inaonesha namna Serikali yetu chini ya uongozi hodari wa Rais wetu unatambua na umedhamiria kuhakikisha wananchi wote wanapata fursa mbalimbali za Uwezeshaji na kuwawezesha kushiriki kumiliki uchumi wa Nchi yao.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Pamoja na jitihada zilizofanyika, bado kuna changamoto ambazo zinaathiri uwezeshaji wananchi na kusababisha mzunguko wa umaskini katika jamii. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Kiwango kidogo cha upatikanaji wa huduma za fedha katika maeneo ya pembezoni na vijijini. Hali hii inakwamisha wafanyabiashara waliowekeza maeneo ya pembezoni na vijijini kushindwa kupanua biashara na wananchi kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

(ii) Ukosefu wa mitaji kwa wananchi wanaohitaji kuanzisha au kukuza biashara kutokana na ukosefu wa dhamana.

(iii) Gharama kubwa ya upatikanaji wa huduma za fedha kutokana na riba kubwa na kufanya gharama kubwa za upatikanaji wa mikopo.

(iv) Ukosefu wa maeneo ya kufanyia biashara yenye mazingira wezeshi kwa ajili ya wafanyabiashara hasa wafanyabiashara wadogo.

(v) Ukosefu wa dhamana kwa wananchi wakiwemo wajasiriamali wadogo na wa kati kutokana na eneo kubwa la ardhi nchini kutopimwa au kurasimishwa. Ardhi ni chombo cha uwezeshaji kwa kutumika kama dhamana ya mikopo.

(vi) Nk

Hivyo sisi kama Baraza tutaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuendelea kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa na fursa mbalimbali za uwezeshaji nchini.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Tunatoa pia shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutenga fedha za Mifuko hii na kuhakikisha uwezeshaji unaendelea kukua. Aidha, tunampongeza kwa kuuboresha Mpango wa Mikopo ya Halmashauri wa 10% na kuweza kuanza tena kwa baadhi ya Maeneo yaliyoainishwa baada ya kusimama kwa muda mfupi kwa ajili ya mapitio.

## HITIMISHO

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Pamoja na changamoto hizi, Maonesho haya yanalenga kuleta matokeo chanya ikiwa ni pamoja na:  kukuza uelewa wa wananchi kuhusu kuwepo kwa mifuko na programu za uwezeshaji; kuwajengea wananchi utamaduni wa kujiwekea akiba na kuwekeza katika miradi ya kiuchumi yenye kuleta faida; na kuongeza hamasa kwa wananchi kutafuta vigezo vya kukopesheka ikiwa ni pamoja na kutumia ardhi kama dhamana na kujiunga kwenye vikundi vya kiuchumi kama SACCOS na VICOBA.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Maonesho haya yamehudhururiwa na **Taasisi mbalimbali zipatazo 50** zikiwemo Mifuko ya Uwezeshaji, Mabenki, Taasisi za Serikali, Taasisi binafsi na Vyuo vya elimu ya kati.

Pamoja na Taasisi hizi tumekuwa pia ushiriki wa **Mikoa 5** ambayo ni Singida, Tabora, Manyara, Shinyanga na Dar es Salaam.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Jumla ya wajasiriamali **zaidi ya 56** na **vikundi 38** wameweza kushiriki kujitangaza na kuuza bishara zao pamoja na kupewa huduma mbalimbali za uwezeshaji ikiwa ni pamoja na: huduma za mikopo nafuu kutoka kwenye mifuko ya Serikali na sekta binafsi; huduma za kibenki na mikopo; elimu ya kodi; elimu ya fedha; elimu ya ufundi; elimu ya kuongeza thamani bidhaa; huduma za bima; huduma za hifadhi ya jamii; elimu ya msambomilia; elimu ya masoko na mitandao ya masoko pamoja na huduma za ithibati ya bidhaa.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Katika Moanesho haya **BRELA** imeweza kusajili majina ya biashara 84, kuhuisha majina ya biashara 7, kutoa leseni 4 pamoja na usajili wa miliki bunifu (IP) 4. **TRA** imeweza kutoa TIN 8, **GS1** imetoa misimbomilia 15,na jumla ya akaunti 139 zimeweza kufunguliwa na Benki zilizoshiriki ambazo ni; CRDB, Azania, NBC,NMB PBZ na TCB.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Katika Kilele cha Maonesho ya Saba ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji pamoja na masuala mengine, ***Mheshimiwa Mgeni Rasmi*** ninakuomba Uzindue mwongozo wa Uratibu na Usimamizi wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji, pia uweze kutoa tuzo kwa Washindi wa Maonesho pamoja na Kutoa mikopo kwa wajasiriamali wachache ambao wamenifadika na baadhi ya Mifuko iliyopo hapa.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Naomba kipekee Nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Halima Dendego; Mkuu wa Mkoa wa Singida kwa namna aliyovyotupokea Mkoani kwake na kuwa na sisi bega kwa bega akiwa na timu yake ya Wakuu wa Wilaya zote pamoja wataalamu wake ili kuhakikisha Maonesho haya yanafanikiwa tena kwa ukubwa na viwango vya juu, ***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Tunashukuru sana.***

***Ninaomba pia kwa mara nyingine niwashukuru wageni waalikwa wote kwa kufika kwenye Kilele cha Maonesho ya Saba ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji. Kipekee nachukua nafasi hii kuwashukuru*** Wadhamini wa Maonesho ya Saba ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji kwa kuwezesha kufanyika kwa Maonesho haya. Huu ni mfano mzuri wa ushirikiano na ninatoa wito kwa wadau wote kujitokeza kwa wingi na kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuwawezesha wananchi. ***Asanteni Sana.***

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

**K**wa kumalizia nawapongeza sana Washiriki wote, wananchi wa Mkoa wa Singida na wadau wote kwa kufanikisha Maonesho ya Saba ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji mwaka 2024. ***Hongereni sana.***

***Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Mgeni Rasmi ninaomba kuwasilisha***

***Nawashukuru Sana kwa Kunisikiliza***